## Vilabu vya Simba, Yanga Sc vyategwa



fikrapevu @fikrapevu @fikrapevu

# BUSATI

Ukweli na Uhakika

Tovuti: www.busati.co.tz | ISSN 3456-3421 Toleo Na.12 Busati Ijumaa Januari 31, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100

### KUINGIZA MATRILIONI KATIKA UMEME...

# Uthubutu wa Dk Samia wapagawisha wengi



>> WAKIRI NCHI SASA ITASONGA MBELE KWA NISHATI YA UHAKIKA

>> WENGI WASEMA BILA NISHATI BORA YA UMEME NI MKWAMO TU

## Unafanya biashara ya Utalii mtaji mdogo?



## Misitu ni zaidi ya uhai wako

# Uthubutu wa Dk Samia wapagawisha wengi

NA CHARLES MATESO

**KITENDO cha Tanzania kuonesha njia katika uwekezaji kwenye nishati ya umeme, imeelezwa ni uthubutu mkubwa ambao umefanywa na Dkt. Samia Suluhu Hassan ambao utaipeleka nchi kwenye neema.**

Wananchi mbalimbali wameendelea kuguswa na kitendo cha Dk. Samia Suluhu Hassan, kuwekeza kwenye nishati ya umeme kwa kutumia kiasi cha Sh trilioni 33 na kusema imegusa maisha ya mamilioni ya Watanzania.

Fedha hizo zitawanufaisha Watanzania wote kwani zinaenda kutibu tatizo la umeme nchini, ambapo kaya zaidi ya milioni 8.3 zitakuwa na uhakika wa kupata umeme na kuondokana na giza.

Wananchi kadhaa waliozungumza na gazeti hili walisema, uhakika wa umeme ni ukombozi kwa kila Mtanzania, kwani kwa dunia ya sasa ya sayani na teknolojia, nishati ya umeme ni kitu cha lazima.

"Hiki kinachokwenda kufanyika ni zaidi ya uwekezaji, wengine wanaweza wasielewe, mfano mimi natoka Mbinga na katika kitongoji chetu hakuna umeme, najua tabu wanazopata wakazi wa pale.

"Nina utaalamu wa mambo ya saluni, lakini nashindwa kufungua chochote kule zaidi ya kukimbia na kuja mjini kuhangaika, huyu Mama (Dkt. Samia), Mungu tu amzidishie," alisema Eva Kapinga mkazi wa Buza, Dar es Salaam.

Katika mahojiano yetu na watu wa kada ya chini na kati, haswa wajasiriamali, walikiri tabu wanayoipata katika umeme wengi hawaijui na wanaweza kusoma katika vitabu au makaratasi na kutoelewa vile wanavyopata shida kwa suala hilo.

"Nipo hapa Masumbwe huku Geita, nimelazimika kuishi katika mji huu maana natoka mbugani (shambani) huko hakuna umeme na tunapata shida, inakuwa tabu kurudi hata nyumbani kuanzisha chochote kile.

"Nilimsikia Mama alichosema, nilijiuliza hii ni ndoto au itakuja kuwa kweli? Yaani anakwenda kutupa raha, anatupa raha ambayo hatunayo kwa sasa,' alisema Maganga Fikiri.

Baadhi ya wachambuzi wa uchumi wameshatamka wazi na kukaririwa wakisifu mpango huo na kusema, uwekezaji unaokwenda kufanyika ni tiba tosha kwa nchi hii.

"Usione vyaelea vimeundwa… hii ndio maana yake, tunataka biashara ya umeme, lazima tuwekeze, nina hakika rais amepata ushauri mzuri ndio maana ameingia kuwekeza, wote walioendelea kwenye biashara hii waliwekeza na rais anawekeza sasa, kupanga ni kuchagua, kama fursa imeonekana kwenye nishati hakuna budi kuitumia.

"Ili uendelee unahitaji kuwa na nishati ya uhakika, nchi zote zenye maendeleo zina nishati ya uhakika na waliwekeza kwenye hilo, uchumi utakua na unajua diplomasia ya uchumi ina nafasi kubwa sana katika kuunganisha mataifa hata Umoja wa Ulaya mambo ya uchumi ndiyo yaliunganisha," alikaririwa mchambuzi wa masuala ya uchumi Walter Nguma.

# Uwekezaji huu utakuwa safi

NA MWANDISHI WETU, Z'bar

**KATIKA kile kile kinachoonekana kujiimrisha zaidi katika uwekezaji Serikali ya Zanzibar, imejipanga kuweka mazingira mauri zaidi katika uwekezaji viiwani humo.**

Hii yote ni kuhakikisha wakazi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla wanafaidika na matunda ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambayo yalikuwa na lengo la kumtoa mwananchji wa kawaida katika ukandamizaji na unyonyaji.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la seMapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amethibitisha hilo na kusema Zanzibar itaendelea kuweka mazingira mazuri zaidi ya kuwavutia wawekezaji zaidi ya uwekezaji hapa nchini.

Rais Dkt. Mwinyi alitoa hakikisho hilo hivi karibuni, wakati alipozungumza na Balozi wa Tanzania nchini, Celestine Kakele aliyefika Ikulu kujitambulisha.

Kutoa hakikisho hilo, Rais Dkt. Mwinyi ameeleza kuwa kuna fursa kubwa ya nchi hizo mbili kushirikiana hasa katika Sekta ya Utalii na Uwekezaji ambazo zikifanyika vyema nchi hizo zinaweza kunufaika kwa kiasi kikubwa.

Dk. Mwinyi amemsisitiza Balozi Kakele kufanya juhudi maalum za kuwavutia wawekezaji kutoka Nigeria kuja kuangalia fursa za Uwekezaji na Serikali inaandaa Mazingira mazuri ya kuwa na Uwekezaji wenye tija na Endelevu.

Amemuhakikishia Balozi huyo kuwa Serikali inaimarisha Uwekezaji kwa kuondoa vikwazo vinavyozorotesha ushirikiano kwa lengo la kuwavutia wawekezaji.

# Nishati mbadala mkombozi wa wengi

NA MWANDISHI WETU

**MKUU wa Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma Mheshimiwa Kapenjama Ndile amewataka wananchi kuachana na matumizi ya kuni na badala yake kutumia nishati mbadala kwa ajili ya kupikia ili kudhibiti uharibifu wa mazingira, kupunguza hatari ya jangwa, na kuhifadhi uoto wa asili.**

Kapenjama amesema haiyo katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Songea (DCC) kilichofanyika katika ukumbi wa HOMSO Songea.

Wadau mbalimbali walihudhuria kikao hicho kwa lengo la kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa kazi kupitia halmashauri za Madaba, Songea, na Manispaa ya Songea.

Miongoni mwa sekta zilizojadiliwa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu matumizi sahihi ya nishati mbadala kama makaa ya mawe, mikakati ya kudhibiti utoro wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari, na udhibiti wa ufugaji holela wa ng'ombe.

Afisa Misitu wa Manispaa ya Songea, Betram Njelekera, amesema kuwa kwa kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini amewezesha vikundi 12 kwa kuwagawia mama lishe mitungi 84 ya gesi ili kusaidia kupunguza uharibifu wa mazingira.



# Biteko anena mitaala ya Teknolojia

NA MWANDISHI WETU

**VYUO na taasisi zinazotoa elimu ngazi ya Kati ikiwemo Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), zimetakiwa kuboresha mitaala yake ya masomo ili iendane na mahitaji ya sasa ya soko la ajira kimataifa sambamba na mahitaji ya kijamii na kiuchumi.**

Hayo yamebainishwa jana na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko katika Maadhimisho ya miaka 60 ya chuo hicho kilichoanzishwa Januari 21, 1965.

"Serikali inasisitiza matumizi ya teknolojia za kisasa na mbinu za kujifunza zinazojibu changamoto za kimataifa, " Amesema Dkt. Biteko.

Amesema kuwa Serikali inazitaka taasisi za elimu ya kati kikiwemo Chuo cha CBE kuweka mkazo kwenye mafunzo ya ujasiriamali, ili wahitimu wake waweze kuchangia kikamilifu katika uchumi wa taifa kupitia biashara bunifu na ajira binafsi.

Aidha, taasisi za elimu, zikiwemo vyuo kama CBE, amezitaka kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira na pia kusaidia kukuza sekta hiyo kwa utafiti na mafunzo.

Ameongeza kuwa, Serikali inahimiza vyuo vya elimu ya biashara kufanya tafiti za kina zinazosaidia kutatua changamoto za kiuchumi, kuimarisha sera za biashara, na kubuni suluhisho endelevu.

"Serikali imeelekeza taasisi kama CBE zihakikishe kwamba fursa za elimu zinafikia makundi yote ya jamii, wakiwemo wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu, ili kuongeza ushiriki wa makundi yote katika uchumi wa taifa," ameongeza Dkt. Biteko.

Naye, Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Selemani Jafo amesema CBE ni kitovu cha biashara nchini na kimeweza kujenga mahusiano na nchi mbalimbali kimataifa ikiwemo nchi ya China na Ujerumani na ni ufunguo wa ufanyaji wa biashara katika kampasi zote nchini.

Kwa upande wake, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba amesema CBE imekuwa ikifanya kazi nzuri na kina mchango mkubwa katika ukuaji wa sekta ya fedha hapa nchini.

"Fedha na Biashara na Uwekezaji havitengamani lakini mafanikio yote yaliyofikiwa lazima tumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono na uongozi wake uliotuheshimisha, " Amesema Mhe. Nchemba.

# Mradi wa maji wapigwa tafu

NA ALBANO MIDELO, Songea

**KATIKA juhudi za kuboresha huduma za maji safi na usafi wa mazingira, serikali ya Tanzania imeanzisha Mradi wa Maji wa Miji 28, ambao unatekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini.**

Mji wa Songea mkoani Ruvuma ni miongoni mwa miji inayonufaika na mradi huu, kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wake.

Mkurungezi wa Mamlaka ya Maji safi Songea (SOUWASA) Mhandisi Patrick Kibasa anasema Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 10 Machi 2023 kati ya Wizara ya Maji na China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kwa gharama ya TZS Bilioni 145.77.

Anasema Utekelezaji wa ujenzi ulianza rasmi Januari 2, 2024, na hadi sasa maendeleo yamefikia asilimia tano

Kulingana na Kibasa Mradi huu umebuniwa ili kuongeza upatikanaji wa maji na kuboresha miundombinu ya maji safi kwa wakazi wa Songea ikiwemo Ujenzi wa miundombinu ya kudaka maji kutoka Mto Njuga katika kijiji cha Kikunja, Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Anasema mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji hadi lita milioni 17 kwa siku.

Kibasa anasema mradi huo unahusisha Ujenzi wa matanki matatu ya kuhifadhi maji yenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni 9. Ujenzi wa matanki haya tayari umeanza na Ujenzi wa mtandao wa bomba za usambazaji maji wenye urefu wa 34.7 km ili kuwafikia wakazi wengi zaidi wa mji wa Songea.

"Mradi pia unahusisha Ujenzi wa mtambo wa kisasa wa kuchuja na kusafisha maji wenye uwezo wa kuchakata lita milioni 16 kwa siku, ili kuhakikisha maji yanakuwa safi na salama kwa matumizi ya binadamu".anasema Kobasa.

Anaongeza kuwa mradi pia unahusisha Ukarabati wa mtambo wa kuchuja na kusafisha maji wa Matogoro, wenye uwezo wa lita milioni 11.5 kwa siku, ili kuboresha huduma za maji safi kwa wakazi wa Songea.

# Wapambanaji kushikwa mkono

NA MWANDISHI WETU

**SERIKALI imekiri bado inaendelea na mpango wa kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora ili kupata masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.**

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe amebainisha mpango wa Serikali katika kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora ili kupata masoko ya uhakika.

Kigahe alisema Serikali imeweka mipango kadhaa ya kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa bora ili kupata masoko ya uhakika ikiwa ni pamoja na kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Hii ikiwa ni kuwasaidia wajasiriamali wadogo kupata maeneo pamoja na majengo ya kuzalishia bidhaa zao, kuwapatia mitaji kupita Mfuko wa NEDF na nembo ya ubora wa bidhaa zao kwa miaka mitatu bila gharama.

Amesema pia kupitia SIDO, TBS na Wakala wa Vipimo (WMA) wataendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali kuhusu kanuni za uzalishaji wenye tija, elimu ya utambuzi wa vifungashio na ufungashaji bora

Pia amesema SIDO kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) itaendelea kuandaa na kuratibu maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwa ni sehemu ya kuchagiza ukuaji wa soko la bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali.

# Ndoto ya Rais Samia kutimizwa katika utalii

**NDOTO ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuongeza idadi ya watalii nchini hadi kufikia milioni tano ifikapo mwaka 2025 na pato la Taifa linalotokana na utalii kufikia Shilingi bilioni sita kwa mwaka, imeshikwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Pindi Chana.**



Juni 7, 2022 Rais Dkt. Samia akiwa kwenye Mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara, aliiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kukutana na wadau wa Sekta ya Utalii kujadili mapendekezo ya mageuzi ya sera, sheria, taratibu na kanuni ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji katika sekta hiyo ili kufikia lengo la kuongeza watalii wanaotembelea nchini hadi kufikia milioni tano, mwaka 2025 sambamba na mapato yatokanayo ya biashara ya utalii.

Katika kutekeleza maagizo hayo ya Rais Dkt. Samia, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ambalo ni muhimili muhimu wa Sekta ya Utalii nchini, limevutia watalii kutoka pande mbalimbali duniani kutembelea Hifadhi za Taifa.

Ukichukua kwa karibu zaidi utaona hadi Aprili 2024, watalii 1,598,608 walitembelea Hifadhi za Taifa. Idadi hiyo ni ongezeko la asilimia 11.4 ikilinganishwa na watalii 1,435,069 waliotembelea Hifadhi za Taifa mwaka wa fedha 2022/2023.

TANAPA imekusanya mapato ya Shilingi 353,441,080,170.15 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 21.58 ikilinganishwa na mapato ya Shilingi 290,698,543,140.17 zilizokusanywa kwa kipindi kama hicho, mwaka wa fedha 2022/2023.

TANAPA chini ya miongozo na maelekezo ya Serikali limeimarisha na kuendeleza miundombinu ya utalii kwa kufungua barabara mpya zenye urefu wa kilometa 694.5 katika Hifadhi ya Taifa Nyerere.

Pia TANAPA imejenga vituo nane vya askari katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Mto Ugalla, Burigi-Chato, Ruaha, Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe na pia limejenga nyumba 29 za watumishi katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Ruaha, Mkomazi, Mto Ugalla, Gombe na Tarangire.

Katika hilo, TANAPA Imekarabati barabara zenye urefu wa kilomita 3,631 katika Hifadhi za Taifa Arusha, Ziwa Manyara, Katavi, Kilimanjaro, Tarangire, Ruaha, Saadani, Burigi-Chato, Mikumi, Rumanyika-Karagwe, Serengeti na Mkomazi pamoja na njia za kupandia milima zenye urefu wa kilomita 157.

TANAPA pia imekarabati viwanja vya ndege 12 katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Serengeti, Katavi, Tarangire na Mkomazi na pia ujenzi unaendelea wa viwanja vya ndege vinne katika Hifadhi za Taifa; Ruaha vipo viwanja viwili, Mikumi kiwanja kimoja na Nyerere kiwanja kimoja.

Kwa upande mwingine, Hifadhi ya Taifa Serengeti imeendelea kupokea tuzo za Africa's Leading National Park inayotolewa na World Travel Awards mara tano mfululizo kuanzia Mwaka 2019, 2020, 2021, 2022 na 2023.

Tuzo nyingine ni Best Nature Destination World 2023 inayotolewa na Trip Advisor, Tuzo ya ubora wa kimataifa inayotolewa na European Society for Quality Research (ESQR) mara nne mfululizo kuanzia mwaka 2020 (Gold category), 2021 (Platinum category), 2022 (Diamond category) na mara nyingine tena 2023 (Diamond category) na tuzo ya Top Attractions kwa Afrika 2023 iliyotolewa na Trip Advisor kwa Hifadhi za Taifa Serengeti na Tarangire.

TANAPA pia inatekeleza miradi 108 ya ujirani mwema katika sekta za elimu, afya, usalama, maji na barabara yenye thamani ya Shilingi bil. 40.7 ambapo Shilingi bil. 36.5 ni kupitia ufadhili wa mradi wa Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) na Shilingi bil. 4.2 kupitia fedha za miradi ya maendeleo.

TANAPA imewezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 74 vinavyopakana na Hifadhi za Taifa Serengeti ni mipango 37, Ziwa Manyara mipango 25 na Tarangire mipango 12.

Ukitazama TANAPA imewezesha vikundi 166 vya kiuchumi vya jamii katika Wilaya za Chamwino ni tisa, Iringa 25, Kilolo tisa, Kilombero 56, Kilosa 15, Mvomero 10, Morogoro 26, Meatu vitatu, Itilima tisa na Busega vinne.



# Tanzania ilivyoibeba Mission 300

**TANZANIA imetajwa kama nchi iliyoonesha njia katika kufikia azma ya kufikisha umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika ifikapo mwaka 2030.**



Hayo yamejiri wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati uliomalizika kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alitajwa katika mkutano huo kama kiongozi mwanamke, wa mfano kwa kuwaunganisha viongozi wenzake barani Afrika na wadau wengine kujadili kwa pamoja mikakati itakayopelekea Bara la Afrika kuwa na nishati ya umeme ya uhakika, endelevu na nafuu.

Rais Samia alisema Bara la Afrika lina jukumu la kuwaondolea umasikini watu wake kwa kufanya uwekezaji na kujenga viwanda vitakavyozalisha ajira na kukuza uchumi. Amesema hayo yatawezekana ikiwa tu, bara la Afrika litakuwa na umeme wa uhakika, endelevu na nafuu.

Kuboresha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini, Rais Samia alisema Tanzania ni moja ya nchi 12 zitakazosaini Mpango Mahsusi wa Kitaifa wa Nishati ambapo Dola za Marekani bilioni 13 zinahitajika katika kipindi cha miaka mitano ijayo ili kutekeza mpango huo.

Kati ya fedha hizo bilioni tano zitatoka sekta binafsi ili kufanya uwekezaji utakaosaidia upatikanaji wa umeme kufikia asilimia 72 ifikapo mwaka 2030.

Rais Samia alisema Serikali yake itatekeleza mpango huo kwa kuongeza uzalishaji wa umeme kupitia vyanzo mchanganyiko na lengo ni kuongeza uzalishaji wa Megawati 2463 kupitia nishati ya jua, gesi asilia, joto-ardhi, upepo na vyanzo vingine ifikapo mwaka 2030.

Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kuunganisha na nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika kwa ajili ya kufanya biashara na nchi hizo. Hadi sasa nchi za Burundi, Rwanda na Kenya zimeunganishwa na Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha umeme na nchi za Zambia na Uganda.

Rais Samia aliongeza kuwa mahitaji ya umeme ya Tanzania kwa sasa ni megawati 1888 na uzalishaji ni megawati 3431, hivyo kuna ziada ya kufanya biashara na nchi nyingine.

Mikakati mingine ni kufikisha umeme kwenye vitongoji baada ya zoezi la kufikisha umeme vijiji vyote vya Tanzania kukamilika na kusambaza nishati safi ya kupikia ambapo malengo ni kuongeza kiwango cha matumizi ya nishati hiyo kutoka asilimia 10 za sasa hadi 80 ifikapo mwaka 2034.

Naye, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt. Akinwumi Adesina ametangaza msaada wa Dola za Marekani bilioni 46 kutoka taasisi mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa Mission300. Fedha hizo zitatolewa na Benki ya Dunia bilioni 22; AfDB bilioni 18; Benki ya Maendeleo ya Kiislam bilioni 2.5; Benki ya Maendeleo ya Uwekezaji wa Miundombinu ya Asia bilioni 1.5; na Mfuko wa OPEC bilioni 2.

Alisema wadau wengine wataendelea kutoa ahadi ya fedha kwa ajili ya kufanikisha mpango huu adhimu kwa maendeleo ya Bara la Afrika.



# Bahari Na Umuhimu Wake

**BAHARI ni rasilimali kubwa na muhimu kwa maisha ya viumbe vyote ulimwenguni. Inachukua zaidi ya asilimia 70 ya uso wa dunia na ina athari kubwa kwa mazingira, uchumi na afya ya binadamu.**

Bahari ni chanzo kikubwa cha maliasili na ina jukumu kubwa katika kudumisha mzunguko wa maji, kudhibiti hali ya hewa na kuchangia katika lishe ya viumbe vyote.

Hapa chini kuna faida na umuhimu wa bahari katika nyanja mbalimbali za maisha ya binadamu na mazingira.

1. Chanzo Kikubwa cha Chakula

Bahari ni chanzo kikubwa cha chakula kwa mamilioni ya watu ulimwenguni.

Inatoa samaki, kamba, kaa, mwani, na aina nyingine nyingi za chakula zinazotegemewa na jamii nyingi kwa lishe.

Samaki wanaopatikana baharini ni chanzo muhimu cha protini na virutubisho vingine, kama vile Omega-3, ambavyo ni muhimu kwa afya ya binadamu.

2. Kudhibiti Hali ya Hewa

Bahari ina mchango mkubwa katika kudhibiti hali ya hewa ya dunia.

Inachukua na kuhifadhi joto kutoka jua, hivyo kusaidia kusawazisha viwango vya joto duniani.

Pia bahari huvuta gesi ya kaboni dioksidi ($CO_2$) kutoka angani na hivyo kusaidia kupunguza gesi chafu inayochangia ongezeko la joto duniani.

Kwa njia hii, bahari husaidia kuzuia athari mbaya za mabadiliko ya hali ya hewa.

3. Chanzo cha Nishati

Bahari ni chanzo kikubwa cha nishati mbadala kama vile nishati ya mawimbi, upepo baharini na nishati ya joto baharini.

Teknolojia hizi zimekuwa zikibuniwa ili kutoa nishati salama na endelevu kutoka baharini, na kwa kufanya hivyo zinapunguza utegemezi wa nishati za kisukuku kama mafuta na makaa ya mawe.

4. Kudumisha Mzunguko wa Maji

Bahari inachangia mzunguko wa maji ulimwenguni kupitia uvukizi, ambao husaidia kuunda mawingu na mvua.

Mvua inayotokana na uvukizi huu ni muhimu kwa kilimo, usambazaji wa maji safi, na maisha ya viumbe vyote duniani.

Mzunguko huu wa maji ni muhimu kwa ajili ya usambazaji wa maji safi na kusaidia kuweka viwango vya unyevunyevu angani.

5. Kusaidia Uchumi wa Jamii za Pwani

Bahari ni chanzo cha ajira kwa mamilioni ya watu katika sekta za uvuvi, usafirishaji, utalii na shughuli za mafuta na gesi.

Jamii za pwani zinategemea bahari kwa ajira na shughuli za kiuchumi zinazosaidia kuinua maisha yao.

Sekta ya utalii, kwa mfano, inaingiza mapato makubwa kutokana na shughuli za utalii wa baharini kama vile kuogelea, kupiga mbizi na michezo ya maji.

6. Chanzo cha Viungo vya Dawa

Bahari ina viumbe na mimea mingi ambayo hutumika katika tiba na utengenezaji wa dawa za kisasa.

Utafiti wa viumbe wa baharini umeonesha kwamba kuna viambato vya kibaolojia katika samaki, mwani na vijidudu vya baharini vinavyoweza kusaidia kutibu magonjwa mbalimbali, ikiwemo kansa, magonjwa ya moyo, na maambukizi.

7. Nyumbani kwa Aina Nyingi za Viumbe

Bahari ni makazi ya aina nyingi za viumbe vya majini kama vile samaki, mamalia wa baharini, matumbawe na viumbe vingine vidogo.

Matumbawe kwa mfano, ni makazi muhimu kwa samaki wengi na ni sehemu muhimu ya mfumo wa kiikolojia wa baharini.

Makazi haya yana umuhimu mkubwa kwa kuendeleza maisha ya viumbe vya baharini na kutunza bayoanuwai (biodiversity).

8. Husaidia Katika Usafirishaji wa Bidhaa

Bahari ni njia kuu ya usafirishaji wa bidhaa duniani, ambapo meli zinatumika kusafirisha bidhaa kutoka nchi moja hadi nyingine.

Usafiri wa baharini ni wa gharama nafuu kuliko usafiri wa anga au nchi kavu kwa bidhaa nyingi na hivyo husaidia kupunguza gharama za usafirishaji na kufanya biashara za kimataifa kuwa za kiushindani zaidi.

9. Husaidia Katika Kupunguza Mabadiliko ya Hali ya Hewa

Bahari huchukua sehemu kubwa ya dioksidi kaboni inayozalishwa na shughuli za binadamu, jambo ambalo husaidia kupunguza kasi ya mabadiliko ya hali ya hewa.



# Misitu ni zaidi ya uhai wako

**MISITU ni rasilimali muhimu sana kwa maisha ya viumbe hai, ikitoa hewa safi, chakula, makazi na kusaidia katika udhibiti wa hali ya hewa.**



Licha ya umuhimu huu uharibifu wa misitu umeleta hasara kubwa kwa mazingira na jamii kwa ujumla.

Kuwepo kwa misitu hutoa faida nyingi, lakini uharibifu wake unasababisha athari mbaya sana.

Katika makala hii, tutaangalia baadhi ya hasara na madhara yanayotokana na misitu kupotea au kuharibiwa.

### 1. Kupotea kwa Makazi ya Wanyama na Viumbe Hai

Kupungua kwa Wanyama wa Porini: Misitu ni makazi ya wanyama wengi, ndege, wadudu, na viumbe vingine. Uharibifu wa misitu unapelekea kupotea kwa viumbe hawa, na baadhi yao hupotea kabisa (kutoweka).

Kuvurugika kwa Mifumo ya Mazingira: Kila kiumbe kwenye msitu kina nafasi yake katika mfumo wa ikolojia. Misitu inapoharibiwa, viumbe wanaoishi huko wanapata changamoto za kuendelea kuishi na kusababisha kuvurugika kwa mfumo wa mazingira.

### 2. Mabadiliko ya Tabianchi

Kuongezeka kwa Joto la Dunia: Misitu husaidia kunyonya hewa ya kaboni ($CO_2$) ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la joto duniani. Misitu inapoharibiwa, gesi za kaboni huachiliwa hewani na kuongeza ongezeko la joto duniani.

Kuvurugika kwa Mvua na Hali ya Hewa: Misitu ina jukumu kubwa katika mzunguko wa mvua. Uharibifu wa misitu unaleta mvurugiko wa mvua, kusababisha ukame au mvua nyingi, na hivyo kuathiri kilimo na maisha ya watu wengi.

### 3. Kuongezeka kwa Erosion ya Udongo

Kupotea kwa Rutuba ya Udongo: Mizizi ya miti husaidia kushikilia udongo na kuzuia mmomonyoko. Misitu inapoharibiwa, udongo unakuwa rahisi kusombwa na maji au upepo, na rutuba hupotea haraka.

Mafuriko na Maporomoko ya Ardhi: Kukosekana kwa miti kumeleta ongezeko la mafuriko na maporomoko ya ardhi katika maeneo yanayokuwa na mvua nyingi. Hali hii husababisha uharibifu wa mali na maisha ya watu.

### 4. Kupungua kwa Rasilimali za Asili

Kupotea kwa Miti ya Matumizi: Misitu hutoa mbao, dawa za asili, matunda, na bidhaa nyinginezo za asili. Uharibifu wa misitu unapunguza upatikanaji wa rasilimali hizi, na kusababisha uhaba kwa watu wanaotegemea misitu kwa maisha yao.

Kupungua kwa Maji Safi: Misitu husaidia kuhifadhi maji ardhini. Misitu inapoharibiwa, chemichemi za maji hupungua, na hali hii huathiri upatikanaji wa maji safi kwa viumbe hai na binadamu.

### 5. Athari kwa Afya ya Binadamu

Kuongezeka kwa Magonjwa: Uharibifu wa misitu unaongeza uwezekano wa magonjwa yanayotokana na mazingira yasiyo safi. Pia, mimea mingi ya dawa hupatikana misituni, hivyo kuharibu misitu kunaweza kupunguza upatikanaji wa dawa za asili.

Kubadilika kwa Mzunguko wa Magonjwa: Baadhi ya wadudu waenezao magonjwa kama mbu wanaweza kuhama kutoka misituni na kuingia kwenye makazi ya watu, hali inayosababisha kuongezeka kwa magonjwa kama malaria.

### 6. Kupotea kwa Utamaduni na Maisha ya Jamii za Kiasili

Kuvurugika kwa Maisha ya Jamii za Wenyeji: Jamii nyingi za asili hutegemea misitu kwa maisha yao. Uharibifu wa misitu unapelekea jamii hizi kupoteza makazi yao, njia za kujipatia riziki, na utamaduni wao.

Kupungua kwa Maarifa ya Kiasili: Jamii za kiasili zinazoishi misituni zina maarifa ya kipekee kuhusu mimea na wanyama. Hivyo, kupotea kwa misitu kunamaanisha kupotea kwa maarifa haya muhimu.

### 7. Hasara za Kiuchumi

Kupungua kwa Ajira: Sekta zinazotegemea misitu kama uchimbaji wa mazao ya misitu na utalii hupata hasara kubwa misitu inapoharibiwa, na kusababisha upungufu wa ajira kwa watu wengi.

Upotevu wa Mapato: Serikali hupoteza mapato yanayotokana na mazao ya misitu kama vile mbao, asali, na mazao ya dawa. Hali hii inazorotesha uchumi wa nchi hasa maeneo yanayotekeleza misitu kwa uzalishaji.

### 8. Kupoteza Hewa Safi

Kusafisha Hewa: Miti huchukua kaboni na kutoa oksijeni ambayo ni muhimu kwa uhai. Uharibifu wa misitu unamaanisha kuwa kuna kaboni nyingi hewani na kiwango kidogo cha oksijeni, hali ambayo ni hatari kwa afya ya binadamu.

Madhara kwa Afya: Pindi msitu unapokatwa na ardhi kuchomwa, moshi unaotokana na uharibifu wa misitu huingia hewani na kusababisha magonjwa ya njia ya hewa kwa binadamu.

### 9. Athari kwa Uchumi wa Dunia

Kupungua kwa Rasilimali za Kibiashara: Uharibifu wa misitu unapunguza upatikanaji wa mbao na bidhaa zingine za kibiashara zinazotoka misituni, hali inayoweza kusababisha upandaji wa bei na kuathiri uchumi wa dunia.

Kupungua kwa Utalii: Misitu huvutia watalii kwa sababu ya uzuri wake wa asili na wanyama. Uharibifu wa misitu hupunguza idadi ya watalii na hivyo kusababisha hasara kwa sekta ya utalii.

### 10. Kuvuruga Mfumo wa Ikolojia

Kupoteza Viumbe Hai: Misitu inapoharibiwa, viumbe hai wengi huathirika kwa kupoteza makazi yao. Kuvurugika kwa mfumo wa ikolojia kunatishia maisha ya mimea na wanyama.

Kubadilika kwa Mizani ya Asili: Misitu husaidia kudhibiti hali ya hewa, kutunza rutuba ya ardhi, na kudhibiti maji. Uharibifu wa misitu unavuruga mizani hii na kuathiri mazingira kwa ujumla.

### Hitimisho

Uharibifu wa misitu una athari mbaya kwa mazingira, jamii na uchumi kwa ujumla.

Ili kudhibiti hali hii, ni muhimu kuhamasisha juhudi za kuhifadhi misitu, kama vile upandaji wa miti, kupunguza ukataji holela wa miti, na kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa misitu.

Kuwekeza katika njia mbadala za kujipatia riziki ambazo haziharibu misitu ni njia bora ya kulinda rasilimali hizi za asili kwa vizazi vijavyo.

# KINACHOTUKIA GOMA, DUNIA IMEJIROGA WAPI?



**INASIKITISHA sana kwa kile kinachoendelea ndani ya Goma mji wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kwa sasa hakuna kinachoendelea zaidi ya risasi na mabomu tu. Dunia imekaa inatazama, nini kinachotukia.**

Je, ni ubinafsi, choyo, tamaa au ulimbukeni? Damu ya watoto wasio na hatia ipo mikononi mwa watu wenye kutaka kufanikisha mambo yao. Ni kilio kitupu.

Wakati mapambano yanaendelea, sasa wataalam wa Umoja wa Mataifa wanatoa uhakikisho kuwa Jeshi la Rwanda linaongoza operesheni za M23, wakielezea jinsi makurutu wa M23 wanavyopewa mafunzo chini ya usimamizi wa Rwanda na kupewa silaha za hali ya juu za nchi hiyo.

Mji wa Goma uko karibu na Ziwa Kivu kwenye mpaka na Rwanda. Huu ni mji mkuu wa Jimbo la Kivu Kaskazini lenye utajiri wa madini na ni kitovu muhimu cha biashara, kituo cha kutoa huduma ya kibinadamu na kituo cha ujumbe mkubwa zaidi wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa.

Jiji hilo pia lilikuwa kimbilio la wale wanaokimbia mzozo kati ya wapiganaji wa M23 na jeshi ambao ulizuka tena mwishoni mwa 2021 na idadi ya watu ikiongezeka hadi karibu milioni mbili.

Wakazi wa jiji hilo wanakabiliwa na hatari zaidi baada ya mapigano kuzuka tena Jumapili usiku. Makabiliano makali yaliyoshuhudiwa yamesababisha maafa yaliyoacha miili ya watu ikiwa imetapakaa mitaani. Hali halisi ya kinachoendelea haijulikani kwasababu mawasiliano ya simu, huduma za umeme na usambazaji wa maji pia imekatizwa. Lakini M23 wanasadikiwa kuteka sehemu kubwa ya jiji hilo.

"Suala la iwapo wanajeshi wa Rwanda kuunga mkono wapiganaji wa M23 ndani ya Goma halina mjadala ," alisema mkuu wa kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Mataifa Jean-Pierre Lacroix, japo aliongeza kuwa ilikuwa vigumu kutaja idadi kamili katika eneo la Goma.

Jumatatu wiki hii baadhi ya wanajeshi wa jeshi la Congo waliokuwa Goma walijisalimisha kwa kuvuka mpaka na kuingia Rwanda.

Tangu mzozo huo uanze, Rais Kagame mara kwa mara amekanusha kuhusika kwa namna yoyote katika kusaidia waasi wa M23, ambao wana vifaa vya kutosha, silaha za kutosha na mafunzo ya kutosha.

Hata hivyo, msimamo huo umebadilika sana huku shutuma zikiendelea kuongezeka huku 'uwezo mkubwa' wa kundi hilo la waasi ukioonyesha uungaji mkono wa Rwanda, kulingana na Richard Moncrief, mkurugenzi wa mradi wa International Crisis Group kwa Maziwa Makuu.

Siku ya Jumapili, Wizara ya Mambo ya Nje ya Rwanda ilisema katika taarifa yake: "Mapigano yanayoendelea karibu na mpaka wa Rwanda ni tishio kwa usalama wa Rwanda, na hivyo basi Rwanda haina budi kujilinda."

Ilisema inasikitishwa na kauli za "kupotosha na za kijanja" zisizo na msingi zinazotolewa kuhusu mzozo huo.

Kwa Kagame, muktadha wa yote haya unatokana na mauaji ya halaiki ya Rwanda ambayo yalifanyika kwa siku 100 mwaka 1994.

Wanamgambo wa kabila la Wahutu waliohusika na mauaji ya hadi watu 800,000 wengi wao kutoka jamii ya Watutsi walikimbilia eneo ambalo sasa ni DR Congo, wengine wakijiunga na Democratic Forces for the Liberation of Rwanda (FDLR).

Kundi hili la waasi bado linafanya kazi katika eneo la mashariki mwa DR Congo ambalo halijatulia - na bado linajumuisha baadhi ya wale waliohusika na mauaji ya halaiki.

Kagame, ambaye aliongoza kikosi cha waasi cha Watutsi ambacho kilimaliza mauaji zaidi ya miongo mitatu iliyopita, anawachukulia "wanamgambo hao wa mauaji ya halaiki" kama tishio lililopo.

Serikali ya Kagame imevamia Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo mara mbili, ikisema inataka kuzuia vikundi vya waasi wa Kihutu kufanya mashambulizi ya kuvuka mpaka.

Mapema Mwezi huu, alimshutumu Rais wa DR Congo, Félix Tshisekedi, kwa kushindwa kushughulikia FDLR na kuzungumza na M23, akisema kuwa hili linazidi kuzidisha mgogoro.

Moncrief anaamini kuwa shambulizi la Goma linahusiana zaidi na kutoa ujumbe wa kisiasa, akisema kuwa M23 halihitaji jiji hilo kimkakati kwani tayari "linadhibiti maeneo mengi yenye faida zaidi."

"Ni njia ya Rais Kagame kuonyesha nguvu yake juu ya nani anayeongoza Kivu Kaskazini," alisema mtaalamu wa Maziwa Makuu.

Rwanda ilimlaumu gavana wa kijeshi wa Kivu Kaskazini, ambaye aliuawa katika mapigano wiki iliyopita, kwa kushirikiana na FDLR.

Wataalamu wanakubaliana kuwa kugundulika kwa ushirikiano wa kiwango cha juu kama huu, ingekuwa kama changamoto kuu kwa Rwanda.

Asili ya M23 inahusishwa na mivutano hii ni kundi la waasi ambalo linasema linapigania maslahi ya jamii ya Watutsi walio wachache mashariki mwa DR Congo.

Uasi wake wa kwanza wa zaidi ya muongo mmoja uliopita ulimalizika kwa makubaliano ya amani - wapiganaji wake walipokonywa silaha na wengi wao wakahamia katika kambi nchini Uganda.

# Unafanya biashara ya Utalii mtaji mdogo?

NA MWANDISHI MAALUM

**UMEANZISHA biashara lakini kwa bahati mbaya kinatukia kitu kibaya zaidi, kile ambacho hata mwenyewe hutaki kukisikia. Yaani hiyo biashara unayoifanya unaikuta katika hali tete, inaenda kufilisika.**



Mbaya zaidi kila ukipiga hesabu unashindwa kuelewa ni kwa nini mambo yamekuwa hivyo, unajaribu kuchanganua kila mahali na kupekenyua kila kitu, ila mwisho wa siku hakuna unachoelewa. Mtaji wako unaenda kuanguka.

Katika makala hii tutajaribu kujifunza kitu kinachoua biashara nyingi. Je unajua ni kitu gani? Karibu sana rafiki tuweze kujifunza.

Waswahili wanasema 'Kukopa Harusi Kulipa Matanga'. Ni mara nyingi sana watu wanapokwenda kukopa huwa wanakuwa na furaha lakini inapofika wakati wa kulipa ndiyo huzuni huanza.

Ukitaka kugombana na kupoteza uhusiano na wateja wako basi anza kuwakopesha. Kukopesha ndiyo kitu kinachoua biashara nyingi na unaweza kuona kuwa usipowakopesha wateja wako utawapoteza katika biashara yako.

Unapokopesha unakuwa huna uhakika na ile hela kwani hela ambayo haiko mikononi mwako siyo ya kuitegemea. Biashara inakuwa haina mzunguko mkubwa wa pesa. Na uhai wa biashara yoyote ni mauzo na kama hakuna mauzo hakuna biashara.

Kwahiyo, kukopesha sana katika biashara yako ni kuua biashara hususani kwa yule mwenye biashara ndogo na mtaji mdogo biashara inakuwa inakosa uhai na hatimaye kufa.

Hatua ya kuchukua na kutambua ni kwamba kukopesha siyo njia ya kumfurahisha mteja, bali ni njia ya kumfukuza na kuvunja mahusiano.

Kwahiyo, kila biashara inahitaji uhai ili iweze kujiendesha na uhai wenyewe ni pesa na pesa inatokana na mauzo. Kama huna mauzo biashara ni rahisi kufa. Hivyo basi, wafanya biashara wengi wadogo wanaua biashara zao kwa njia ya kukopesha huku wakiamini wanamfurahisha mteja.

Mfumo wa biashara unafanya kazi kama vile mwili wa binadamu unavyofanya kazi. Mwili wa binadamu ukikosa damu basi binadamu naye ataweza kufa. Vivyo hivyo kwa biashara kama imekosa fedha za kujiendesha lazima itakufa pia kama ilivyo katika mwili wa binadamu.

Kuna kitu ambacho wafanyabiashara wengi wanafanya wakijua kuwa wanawafurahisha wateja kumbe ndiyo wanawafukuza wateja.

Usipowajua watu vizuri katika biashara yako watakusumbua hivyo unatakiwa kuijua biashara yako vizuri na kuwajua wateja wako vizuri na kuwapatia huduma bora kabisa ambayo hawatoweza kuipata sehemu nyingine yoyote ile.

Kuna sumu ambayo inaua biashara nyingi, inafanya biashara ife mapema kwa kukosa fedha za kujiendesha yenyewe. Rafiki, mkopo katika biashara ndiyo sumu namba moja ya kumfukuza hata mteja wako kama huliamini hilo jaribu katika biashara unayofanya.

Watu wanakawaida kujisikia uchungu kutoa hela ambayo tayari wameshapatiwa huduma anakuwa hakuna kinachomsukuma kwa sababu kile ambacho ana kitaka tayari amekipata.



# Vuta watalii mtandaoni, ila zingatia hili

**VITU vya kuzingatia unapofanya biashara mtandaoni Tanzania ni muhimu kufahau mapema kwasababu Kufanya biashara kwenye mtandao ni jambo lenye faida na changamoto zake.**

Unaweza ukawa na bidhaa nzuri sana lakini ukumbuke kuwa kila siku kunaanzishwa tovuti za kuuza bidhaa mtandaoni.

Haijalishi kuwa wewe ni muuzaji wa bidhaa wa siku nyingi au wa karibuni, ni wazi kuwa utakutana na changamoto kadha wa kadha.

**Jitahidi Kukosa Wateja**

Ni rahisi mtu kukaa dukani kwake siku nzima ili kuwahudumia wateja; lakini unaona hakuna umuhimu wa kukaa karibu na wateja wake wa kwenye mtandao.

Kumbuka hawa ni wateja kama wateja wengine, wanaweza kuwa wana maswali, maombi au mapendekezo wanayotaka kuyafikisha kwako.

Wateja watakufikia vipi na wewe hujaweka mfumo mzuri wa huduma kwa wateja? Je watanunua tu vitu kwa sababu unapenda wanunue? La hasha! Kutokana na kosa hili hutoweza kupata wateja na kufanikiwa katika biashara yako.

**Epuka Kutengeneza Website Mbaya**

Katika jambo muhimu kwenye biashara ya kwenye mtandao ni tovuti iliyotengenezwa au kusanifiwa vizuri. Watu wengi hutengeneza tovuti mbaya ambazo siyo rafiki kwa wateja na vifaa vyao.

Hili huwagharimu wengi kwa kupoteza wateja wengi. Zingatia mambo haya katika kutengeneza tovuti nzuri ya kufanyia biashara ya kwenye mtandao:

Hakikisha inaweza kuonekana vyema kwenye vifaa vyote kama vile simu, tablet na kompyuta.

Hakikisha ina mfumo mzuri wa viungo (Menu and Navigation) kwa njiaa hii mteja ataweza kuperuzi vyema kwenye tovuti yako. Hakikisha inasehemu ya utafutaji.

Ukizingatia mambo haya tovuti yako itakuwa nzuri kwa wateja na kukufanya kupata mauzo zaidi.

**Epuka Ufafanuzi Mbovu wa Bidhaa**

Hakuna mtu anayenunua kitu ambacho hajakifahamu vizuri au kukiona. Kosa la ufafanuzi au maelezo duni ya bidhaa limewafanya wateja wengi kutonunua bidhaa za wafanya biashara wengi.

Hakikisha bidhaa ina picha nzuri na maelezo ya kutosha kumfanya mteja aielewe bidhaa yako ili awe tayari kuinunua.

Kwa mfano mtu unaweka picha ya bidhaa fulani kwenye tovuti au mtandao wa kijamii bila hata maelezo yoyote, je unafikiri kwa sababu umeiweka kama cover au profile picture ndiyo itanunuliwa? Ni lazima watu wapate maelezo ya kutosha na jinsi bidhaa husika itakavyowasaidia ndipo watainunua.

**Jitahidi Kutumia Mitandao Ya Kijamii**



Wafanya biashara wengi hawajui umuhimu wa mitandao ya kijamii wala matumizi yake kwenye biashara zao.

Biashara ya kwenye mtandao inahitaji ufahamu matumizi mazuri ya mitandao ya kijamii ili kupata wateja wengi zaidi kwa ajili ya bidhaa zako.

Hakikisha unawajulisha watu jinsi bidhaa zako zitakavyotatua matatizo yao pia usisahau kuwajulisha punguzo (offer), bei na njia ya kuzipata bidhaa zako.

**Epuka Kutokufahamu Wateja, Soko Lako**

Kufahamu wateja na soko ni hatua mojawapo ya kukuwezesha kukuza mauzo ya bidhaa zako.

Hebu fikiri unatangaza bidhaa za urembo za wanawake kwenye group la wa Whatsapp, je utapata wateja kweli? Naamini hutopata wateja jinsi ipasavyo.

Ni wazi kuwa ni muhimu ujue soko lako liko wapi na ulilenge ipasaavyo.

**Epuka Mfumo Mbovu wa Kulipia Bidhaa**

Mara nyingi unapouza vitu kupitia mtandao wateja watalipia bidhaa zao moja kwa moja, pia watafahamu jisi watakavyopata bidhaa husika.

Wauzaji wengi hawaweki mfumo rahisi kwa wateja ili waweze kufanya malipo kwamfano tovuti za Afrika Mashariki tunategemea kuona njia za malipo kwa njia za mtandao.

Pia ni lazima kuwe na mfumo mzuri wa kuwasafirishia au kuwafikishia wateja bidhaa zao. Kwa kufanya hivi utaaminika zaidi na kujiongezea wateja

**Jitahidi Kutatua Matatizo Kuliko Kuuza Bidhaa**

Mara nyingi nimekuwa nikisisitiza kuwa pesa ni matokeo ya kutatua shida za watu.

Pamoja na kulenga kuuza bidhaa zako na kupata pesa, ni lazima kwanza uhakikishe unatatua matatizo ya watu kupitia bidhaa zako kwanza.

Ni muhimu pia kujenga imani kwa wateja kwa kuwapa garantii na punguzo (offer) kwa ajili ya bidhaa zako.

Kwa kufanya hivi utaongeza imani ya watu kwenye bidhaa na biashara yako.

**Jitahidi Kujitangaza Zaidi**

Biashara ni matangazo Jinsi matangazo yalivyo muhimu katika biashara za aina nyingine, ndivyo ilivyo pia kwenye biashara ya kwenye mtandao.

Ni lazima utumie njia mbalimbali za kuzitangaza bidhaa zako, ukihusisha njia za bure na zile zakulipiwa.

Kwa njiaa hii utawezakutambulika kati ya washindani wako, hivyo kufikia wateja wengi zaidi.

Kamwe usifanye kosa la kuupuuzia matangazo kwenye biashara ya kwenye mtandao kwani kuna ushindani mkubwa.

# Umuhimu wa Wanyama Pori Tanzania

**WANYAMA pori ni viumbe wanaoishi katika mazingira yao asilia bila kufungwa na binadamu. Hawa ni pamoja na aina nyingi za mamalia, ndege, reptilia, na wadudu ambao wanapatikana katika misitu, savanna, milima, mabonde na hata katika maeneo ya maji kama mito na bahari.**



Wanyama pori wana mchango mkubwa sana kwa mazingira, uchumi, na jamii kwa ujumla.

Kutambua faida na umuhimu wa wanyama pori ni muhimu katika juhudi za kutunza na kulinda maliasili hizi muhimu.

**1. Faida na Umuhimu wa Wanyama Pori kwa Mazingira**

Uhifadhi wa Mazingira na Mnyororo wa Chakula

Wanyama pori husaidia kuimarisha mfumo wa ikolojia kwa kudhibiti idadi ya viumbe mbalimbali katika mnyororo wa chakula.

Kwa mfano, wanyama walaji-nyasi (herbivores) kama nyati na pundamilia hula nyasi na kupunguza msongamano wa mimea, hivyo kusaidia katika kudhibiti ukuaji wa mimea.

Wanyama wanaokula nyama (carnivores) kama simba na chui husaidia kudhibiti idadi ya wanyama wanaokula nyasi, na hii inasaidia kuhifadhi uwiano katika mazingira.

**Kusaidia katika Usambazaji wa Mbegu**

Wanyama pori kama tembo, ndege, na wadudu husaidia katika usambazaji wa mbegu za mimea wanapohama kutoka eneo moja kwenda jingine.

Hii ni muhimu kwa kuendeleza msitu na kuimarisha uoto wa asili katika maeneo mbalimbali ambayo nayo husaidia kuhifadhi rutuba ya ardhi na hewa safi.

Kuhifadhi Ubora wa Udongo

Baadhi ya wanyama pori kama vile wadudu wa ardhini huchangia katika kuongeza rutuba ya udongo kwa kuchimbua na kuchanganya udongo.

Hii inasaidia mimea kukua kwa urahisi na kudumisha uzalishaji wa chakula katika ikolojia ya asili.

Kuzuia Athari za Mabadiliko ya Tabianchi

Msitu na maeneo yenye mimea mingi ambayo yanatunzwa na wanyama pori yanaweza kufyonza dioksidi kaboni ($CO_2$) kutoka angani.

Wanyama pori, hasa wale wanaosaidia ukuaji wa msitu, husaidia katika kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuhifadhi hewa safi na kupunguza uzalishaji wa gesi zinazochafua mazingira.

**2. Umuhimu wa Wanyama Pori kwa Uchumi**

Sekta ya Utalii wa Wanyamapori

Nchi nyingi, hasa katika Afrika, hutegemea utalii wa wanyama pori kama chanzo kikuu cha mapato.

Watalii kutoka nchi mbalimbali huja kushuhudia uzuri wa wanyama pori kama vile tembo, twiga, simba, na faru.

Hii inachangia mapato kupitia ada za kuingilia hifadhi, malazi, na usafiri.

Mapato haya yanasaidia serikali na jamii katika kujenga miundombinu na huduma za kijamii.

**Kazi na Ajira kwa Wenyeji**

Utalii wa wanyama pori huunda nafasi nyingi za ajira kwa wenyeji kama vile waongozaji wa watalii, walinzi wa wanyama, wapishi na wafanyakazi wa hoteli.

Hii inasaidia kuboresha maisha ya jamii zinazozunguka hifadhi za wanyama pori na kusaidia kuboresha uchumi wa eneo husika.

**Chanzo cha Vyakula vya Asili**

Jamii zingine hutegemea wanyama pori kama chanzo cha vyakula vya asili, ingawa hili linapaswa kufanywa kwa kuzingatia sheria na kanuni za uhifadhi.



# Mambo 10 ya Kushangaza Israeli-2

**ISRAEL ni nchi ambayo mara nyingi inagonga vichwa vya habari kwa umuhimu wake wa kihistoria na mazingira ya kisiasa. Hata hivyo, kando na hadithi zinazofanya habari za kimataifa, kuna mambo mengi ya kuvutia ya taifa hili ndogo lakini yenye utofauti wa ajabu ambayo hayajulikani sana.**



Kutoka kwa uvumbuzi wake wa kiteknolojia hadi muundo wake wa kitamaduni tofauti, Israeli imejaa mshangao. Hapa kuna mambo kumi ya kushangaza kuhusu nchi hii ya kipekee.

Endelea…

**5. Chungu Kiyeyuko cha Vyakula vya Ulimwenguni**

Eneo la upishi la Israeli ni tofauti kama wakazi wake, linatoa mchanganyiko wa ladha kutoka duniani kote. Chungu cha kuyeyuka cha vyakula vya kimataifa, chakula cha nchi hiyo kimeathiriwa na vikundi vingi vya wahamiaji ambavyo vimehamia Israeli, kila kimoja kikileta mguso wake wa kipekee kwenye meza.

Kuanzia vyakula vya kupendeza vya Ulaya Mashariki hadi nauli ya viungo vya Afrika Kaskazini na kila kitu kilicho katikati, vyakula vya Israeli ni karamu ya kweli kwa hisi.

Zaidi ya hayo, uvumbuzi wa upishi wa Israeli hauishii katika mapishi ya jadi. Wapishi wa Israeli wanajulikana kwa ubunifu wao wa vyakula vya asili, na hivyo kusababisha hali ya chakula inayobadilika na inayozidi kutambulika kimataifa. Migahawa katika miji kama Tel Aviv na Jerusalem mara nyingi husifiwa kwa menyu zao bunifu ambazo huchanganya viambato vya kitamaduni na mbinu za kisasa, na hivyo kuunda hali ya matumizi ya chakula ambayo ni ya kipekee ya Waisraeli.

6. Idadi ya Makumbusho yenye Rekodi

Licha ya ukubwa wake mdogo, Israeli inajivunia idadi kubwa zaidi ya makumbusho kwa kila mtu ulimwenguni. Kupitia masomo mbalimbali, kuanzia sanaa na historia hadi sayansi na teknolojia, makumbusho ya Israeli huhifadhi na kusherehekea urithi wa kitamaduni na uvumbuzi mbalimbali wa taifa.

Kwa mfano, Jumba la Makumbusho la Israel huko Yerusalemu, lina mkusanyiko mkubwa unaotia ndani akiolojia, sanaa nzuri, na sanaa na maisha ya Kiyahudi.

Wingi wa makumbusho ni onyesho la shukrani ya kina ya watu wa Israeli kwa historia, utamaduni, na kujifunza. Zinatumika kama njia ya elimu, mazungumzo na maelewano kati ya raia wa nchi na wageni wake.

Kwa maonyesho ambayo yanalenga ndani na nia ya kimataifa, taasisi hizi hutoa dirisha katika tabaka nyingi za zamani na sasa za Israeli.

**7. Kalenda ya Kipekee ya Israeli**

Mchanganyiko wa Kalenda za Israeli hufanya kazi kwenye kalenda ya kipekee inayochanganya kalenda ya kiraia ya Gregorian na kalenda ya jadi ya Kiebrania inayotegemea mwezi. Mfumo huu wa pande mbili una jukumu kubwa katika maisha ya Waisraeli, haswa kuathiri sikukuu za umma na maadhimisho ya kidini. Ingawa ulimwengu wa biashara kwa ujumla hufuata kalenda ya Gregorian, likizo na mila za Kiyahudi hufuata kalenda ya Kiebrania, ambayo imekuwa ikitumika kwa milenia.

Kusukwa kwa kalenda hizi kunasisitiza dhamira ya Israeli ya kuunganisha mila na jamii ya kisasa. Inaonyesha jinsi desturi za kale zimeunganishwa katika maisha ya kisasa ya Israeli.

Mpangilio huu wa kalenda mbili pia huathiri ratiba za kila siku, nchi inapojitayarisha kwa ajili ya likizo kama vile Pasaka, Yom Kippur, na Hanukkah, ambazo huwa katika tarehe tofauti za Gregorian kila mwaka.

**8. Mahali Patakatifu kwa Viumbe vilivyo Hatarini Kutoweka**

Israeli ni nyumbani kwa hifadhi kadhaa za asili na mbuga za kitaifa ambazo hutumika kama mahali pa kuhifadhi wanyama walio katika hatari ya kutoweka.

Eneo la kijiografia la nchi, kwenye makutano ya mabara matatu, huipa bioanuwai ya kipekee, huku mamia ya spishi za ndege wakipitia wakati wa kuhama kwao kwa msimu. Juhudi za uhifadhi nchini Israeli ni muhimu sana kwani zinasaidia kulinda viumbe adimu kama vile Oryx ya Arabia, ambayo imerudishwa tena porini baada ya kukaribia kutoweka.

Mipango hii ya mazingira inaangazia dhamira ya Israeli katika kuhifadhi ulimwengu wa asili. Kupitia usimamizi makini na kuzingatia uendelevu, Israel inachangia kikamilifu katika juhudi za uhifadhi wa kimataifa. Zaidi ya hayo, makazi mbalimbali ya nchi, kutoka kaskazini mwa nchi kavu hadi kusini kame, hutoa mazingira bora kwa aina mbalimbali za viumbe ili kusitawi.

**9. Wajibu wa Kushangaza wa Israeli katika Ulimwengu wa upishi**

Zaidi ya eneo lake la upishi, Israeli ina jukumu kubwa katika tasnia ya chakula ulimwenguni, haswa katika uwanja wa teknolojia ya chakula na uvumbuzi.

Makampuni na watafiti wa Israeli wako mstari wa mbele katika kutengeneza protini mbadala, teknolojia za kilimo, na suluhu zenye msingi wa lishe ili kulisha idadi ya watu inayoongezeka duniani kwa njia endelevu...**itaendelea**

# Pambana ili utajirike, usilale




**KUNA wakati jarida maarufu la Forbes ilizua maoni mengi wakati lilipodai mmoja kati ya watu nyota kwenye mitandao ya kijamii kwa wakati huo, Kylie Jenner amepata utajiri wa karibu Dola bilioni 1.**

Haya ni mafanikio ambayo watu wachache sana wanaweza kuyapata na kulikuwa na watu 5,700 kote duniani waliokuwa na utajiri unaozidi dola milioni 500 2017 kulingana na ripoti kutoka kwa Global Wealth Report.

Mabilionea halisi hata hivyo ni wachache. Lakini mtu anahitaji nini hadi kuitwa bilionea?

### ANZISHA KAMPUNI

Ukiangalia watu matajiri duniani kwa mfano Jeff Bezos wa Amazon, Mark Zuckerberg wa Facebook, Amancio Ortega wa Zara na Jack Ma wa Alibaba ndio wanatawala.

Forbes inawatambua watu thuluthi mbili ya mabilionea 2,208 kuwa waliojizolea utajiri wao na idadi hiyo inazidi kuongezeka.

Kylie Jenner kumshinda Mark Zuckerberg kwa kasi ya utajiri

Ni kweli kuwa neno utajiri wa kujizolea linaweza kuwa na ugumu kulielezea. Hatua ya Forbes kumtaja Kylie Jenner ambaye alizaliwa katika familia tajiri kama aliyejipatia utajiri ilizua maoni mengi kwenye mtandao.

### PESA ZA URITHI

Karibu theluthi moja ya watu walio katika orodha ya Forbes walirithi pesa zao.

Hao ni pamoja na watu saba wa familia ya Walton, warithi wa maduka wa Walmart na Francoise Bettencourt-Meyers ambaye familia yake ilianzisha kampuni ya L'Oreal.

Mwanzilishi wa Amazon sasa ndiye mtu tajiri dunia. Urithi ni muhimu hasa barani Ulaya kutokana na kuwa umechangia kwa karibu nusu ya mabilionea kulinda na takwimu za Forbes za mwaka 2014.

Kuna sababu kadhaa zilizochangia watu ambao walirithi mali kuzidi kuongezeka.

Sababu moja ni kuwa thamani ya mali kama hisa imeongezeka kwa haraka kuliko mali nyingine miaka ya hivi karibuni.

### WEKEZA

Kuna zaidi ya watu 140 katika sekta ya fedha walio na utajiri unaozidi dola blioni 2.5 kwenye orodha ya watu matajiri.

Bill Gates alichukua tena uongozi wa kuwa mtu tajiri duniani na wengi wao ni kutoka nchini Marekani ambapo asilimia 25 ya mabilionea hupata utajiri wao kutoka sekta ya fedha.

Lakini usidhani kuwa ni rahisi kupata mafanikio hayo. Mkuu wa kampuni ya JP Morgan Chase boss Jamie Dimon ni baadhi ya mabilionea wachache waliochukua mkondo huo. Na wafadhili wengi karibu asilimia 20 ya watu matajiri zaidi ya 143 wana uhusiano na mifuko ya uwekezaji.

### HAMA ULIPO

Idadi ya mabilionea katika kila nchi inashuka, ila eneo linaloongezeka kwa watu matajiri duniani ni la Asia Pacific.

Karibu asilimia 29 ya watu mabilionea wapya mwaka uliopita walitokea eneo hilo kwa mujibu wa jarida la WealthX linalokadiria kuwa kuna mabilionea 2,750 duniani idadi iliyo juu kuliko ile ya Forbes.

China pekee ina mabilionea 29 kati ya 259 mabilionea wapya, idadi ya juu kuliko ya nchi yoyote.

Licha ya hatua zilizopigwa sehemu zingine duniani, Marekani inasalia nchi yenye mabilionea wengi zaidi ikiwa na mabilionea 585.

### USIWE MTU WA KESI

Mabilionea si wageni kwa kesi mahakamani. Kwa mfano Bill Gates, anaweza kujulikana kama mtu tajiri wa kutoa misaada lakini historia yake si safi vile.

Mnamo miaka ya tisini Marekani iliishtaki kampuni ya Microsoft kwa kutumia mbinu zinazozuia ushindani.

Serikali ya Marekani ilishinda na Microsoft ikakata rufaa. Kesi hiyo iliishia makubaliano. Tume ya Ulaya nayo ishaipiga faini kampuni ya Microsoft.

Baadhi ya kampuni ambazo pia zimepigwa faini ni pamoja na Google na Samsung na pia zile zisizo za teknolojia kama ya kamari ya Las Vegas Sands.



# Wachezaji waliowahi kunangwa na makocha wao



**KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim amegonga vichwa vya habari aliposema, ni bora kumuweka kama mchezaji wa akiba kocha wake wa makipa mwenye umri wa miaka 63, kuliko Marcus Rashford, kwa sababu hana juhudi.**

Rashford hajacheza kwenye kikosi cha United kwa muda wa wiki sita. Amorim anasema mshambuliaji huyo wa Uingereza hafanyi vyema katika mazoezi.

Mustakabali wake ndani ya Old Trafford haujulikani. Kuna klabu za Ulaya zinazohusishwa na kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho wa wachezaji wiki ijayo.

Sio mara ya kwanza kwa kocha wa Ligi Kuu England kumkosoa hadharani mmoja wa wachezaji wake.

### Harry Redknapp na Darren Bent

Harry Redknapp alidai kuwa mke wake angefunga, pale Darren Bent alipokosa bao dakika za lala salama. Siku Tottenham ilipotoka sare ya 1-1 na Portsmouth Januari 2009.

Redknapp alisema: "Huwezi kupata nafasi nzuri zaidi ya kushinda goli kuliko ile uliyoipata. Hata mke wangu angeweza kufunga."

Licha ya kauli hiyo, Bent alibaki kwenye safu ya wachezaji wa Redknapp na alimaliza msimu wa 2008-09 kama mfungaji bora wa Tottenham akiwa na mabao 17, kabla ya kujiunga na Sunderland majira ya kiangazi.

Redknapp alitumia miaka mingine mitatu na nusu akiwa White Hart Lane (Tottenham) akiwasaidia kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa mwaka 2011, lakini alitimuliwa Juni 2012.

### Harry Redknapp na Adel Taarabt

Redknapp, wakati huo akiwa meneja wa QPR, hakusita kumkosoa Adel Taarabt alipoulizwa kwa nini kiungo huyo ameachwa nje ya kikosi kwenye mchezo dhidi ya Liverpool, Oktoba 2014.

"Siwezi kuwalinda watu ambao hawataki kukimbia na kufanya mazoezi, na wana uzito wa mawe matatu," alisema Redknapp.

"Alicheza katika mchezo wa timu ya kikosi cha pili juzi na ningeweza kukimbia zaidi ya alivyokimbia yeye. Siwezi kumchagua."

Taarabt ilijibu kwa kusema Redknapp alikuwa akitoa visingizio kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo, wakati huo timu ikiwa nafasi ya chini kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Kiungo huyo aliichezea klabu hiyo mechi tano tu, kabla ya kujiunga na Benfica msimu wa joto wa 2015.

QPR ilishuka daraja mwishoni mwa msimu wa 2014-15. Redknapp aliipandisha tena daraja timu hiyo msimu uliofuata kabla ya kung'atuka Januari 2015.

### Jose Mourinho na Luke Shaw

Jose Mourinho alimkosoa beki wa Uingereza, Luke Shaw wakati akiinoa Manchester United, akihoji kujitolea na utimamu wake.

Baada ya kuingia kama mchezaji wa akiba dhidi ya Everton Aprili 2017 Mourinho alisema beki huyo wa pembeni alitumia "mwili wake na ubongo wangu."

Aliongeza: "Alikuwa mbele yangu na nilikuwa nikimfanyia kila uamuzi."

Shaw bado yuko Old Trafford lakini ana jeraha, na amecheza mechi tatu tu msimu huu. Mourinho alifutwa kazi Disemba 2018 baada ya kuuanza vibaya msimu huo.

### Jose Mourinho na Tanguy Ndombele

Mourinho, alihamia Tottenham na kuwa meneja wa Tottenham, alimkosoa mchezaji aliyesajiliwa kwa pauni milioni 54, Tanguy Ndombele, Machi 2020.

Baada ya kiungo huyo kubadilishwa wakati wa mapumziko ya mchezo dhidi ya Burnley, Mourinho alisema: "Kipindi cha kwanza hatukuwa na safu ya kiungo. Yeye (Ndombele) amepata muda wa kutosha kupanda kiwango.

"Najua Ligi Kuu ni ngumu, na wachezaji wengine huchukua muda mrefu kuzoea ligi tofauti. Lakini mchezaji mwenye uwezo kama yeye, ni lazima atupe zaidi ya anachotupa sasa."


BUSATI
# MICHEZO
fikrapevu @fikrapevu @fikrapevu
Ijumaa Januari 31, 2025
Tovuti: www.tanzan .tz



# SIMBA, YANGA ZATEGWA

NA MWANDISHI WETU

**FAHAMU kwamba mwenye kucheza na kutoa maelekezo ndani ya kikosi cha Yanga, Pacome Zouzoah ni pasua kichwa kutokana na uwezo wake kwenye kupiga pasi ndefu na fupi akiwa uwanjani.**



Nyota huyo kwenye dirisha dogo ilikuwa inatajwa kuwa yupo kwenye rada za mabosi wa Simba kwa kuwa mkataba wake unagota mwisho inaelezwa kuwa mabosi wa Yanga walifanya mazungumzo naye kuhusu kuboresha mkataba wake.

Hivi karibuni Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally aliweka wazi kuwa wanamfuatilia mchezaji huyo kwa kuwa wanatambua mkataba wake unakaribia kuisha wakiona anafaa watahangaika naye.

“Kuna mchezaji ambaye yupo pale ambaye ni Pacome huyu tunamfuatilia tukiona anatufaa basi tutahangaika naye kwa kuwa tunajua kwamba mkataba wake unaisha.”

Pacome ndani ya ligi amecheza jumla ya mechi 14 kati ya 15 akikosekana kwenye mchezo mmoja akisepa na dakika 803 uwanjani akifunga mabao 5 na kutoa pasi tatu za mabao.

Yanga kwa sasa ipo kwenye maandalizi kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Kagera Sugar mchezo unaotarajiwa kuchezwa Uwanja wa KMC, Complex, Februari Mosi 2025.